Usawiri wa Jinsia katika Lugha Mwiko na ya Tasfida Miongoni mwa Jamii ya Ameru, Kenya

Douglas Nkumbo, James Ogola Onyango, James Gwachi Mayaka
Laikipia University, Kenya

Abstract
Do taboo words and euphemisms serve any sociall purpose or are they just lyrics of old folk? Members of a society experience difficulties when using taboo words so they resort to using euphemism. Various studies have revealed that language use depict some gender biases. This study was purposed to explore the use of taboo words and euphemism in Kimeru language and show how these linguistic items portray gender. The objectives of this study were to identify taboo words and euphemistic words in relation to private body parts and the acts of sexual intercourse, and to analyze how euphemistic words depict gender within Ameru community. On the research methodology, the researcher used questionnaire, participatory method and interviews to collect data. Twenty five taboo words and fifty euphemism words were analyzed in light of hegemonic masculinity. The findings of this study indicated that there are taboo words in Kimeru language used in various settings which are used from a euphemistic perspective. Euphemistic words portray men positively and women negatively thus showing men dominance over women. The researcher used simple calculation of various taboo and euphemistic words to show their frequency modes. The researcher used description and tables to analyze and represent the data collected. The results of the study should be very instrumental to other researchers, students of language and culture, journalist and gender activists in their campaigns for equality.

Keywords: Gender, euphemism, hegemonic masculinity, portrayal, taboo words.

Ikisiri
Ingawa lugha ni muhimu katika mawasiliano, tafiiti mbalimbali zimedhihirisha jinsi lugha hutumika kusawiri jinsia, utafiti huu uliangazia jinsi lugha ya tasfida inavyosawiri jinsia katika jamii ya Ameru. Wanajamii hupata ugumu kuzungumzia maswala ambayo yanahusiana na namna ya kurejelea: Sehemu za siri, tendo la ngono na majukumu ya sehemu za siri kwani mada kama hizi ni mwiko katika jamii nyingi ilhali zinatuhusu kila siku. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni: kubainisha istilahi za mwiko na za tasfida katika jamii ya Ameru, kuonyesha miktadha ya matumizi ya lugha mwiko na ya tasfida katika jamii ya Ameru na kutathmini namna jinsia inavyosawiriwa kupitia lugha mwiko na lugha ya tasfida katika jamii ya Ameru. Mbinu za utafiti zilizotumika ni: Matumizi ya hojaji ambapo wanawake kumi na wanaume kumi kati ya umri wa miaka kumi na nane hadi hamsini walijaza hojaji, uchunguzi shiriki na mahojiano ya ana kwa ana. Utafiti ulitumia istilahi ishirini na tano ambazo ni mwiko na istilahi hamsini za tasfida ambazo hurejelea mada hizi. Nadharia iliyotumika ni nadharia ya uwezo uume. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha jinsi mwanamke anavyodunishwa kupitia kwa lugha mwiko na ya tasfida naye mwanamume anatukuzwa. Utafiti ulitumia maelezo na jedwali kuchanganua na kuwasilisha data kwa kuonyesha: Umaratokezi wa kila istilahi, jinsia inayotumia na umri wa wanaotumia. Utafiti una matumiani kuwa, matokeo yake yatasadia katika usomi wa lugha, jinsia na utamaduni pamwe na watetezi wa usawa wa kijinsia katika jamii.

Maneno muhimu: Jinsia, lugha mwiko, tasfida, uwezo kiume, Usawiri.

Utangulizi

Wameru ni nasaba ya Wabantu, wanaoishi nchini Kenya katika kaunti ya Meru na Tharaka-Nithi. Kuna lahaja saba za Kimeru: Kitigania, Kiimenti, Kitharaka, Kigembe, Kichuka, Kimuimbi na Kiigoji.Wameru wote wana utamaduni sawa.

Jamii ya Ameru ni ya kuumeni, hivi kwamba mwanamume hupewa hadhi ya juu kuliko mwanamke. Mwanamume ndiye mkuu wa familia na uamuzi wote wa maswala ya kifamilia na ya kijamii humtegemea yeye. Mwanamke hujitokeza kama msaidizi tu.

Taswira ya mwanamume katika jamii za Kiafrika ni swala ambalo limeibua changamoto katika mijadala na makongamano mbalimbali, hasa kwa misingi ya uhalisia wa nadharia tete ya uwezo uume. Tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiafrika humsawiri mwanamume kwa njia tofauti na mwanamke.Tafiti nyingi zimefanywa katika jamii mbalimbali kwa kuzingatia tanzu mbalimbali za fasihi hasa kwa kuangaza sura ya mwanamke na matokeo yake ni kwamba mwanamke hutwezwa ilhali mwanaume hutukuzwa. Kwa mujibu wa utafiti huu tulidhamiria kutumia utanzu wa isimu kudhihirisha iwapo maneno ya mwiko na ya tasfida humtweza mwanamke na kumtukuza mwanamume.

Yalioandikwa Kuhusu Mada hii

Wanaisimu mbalimbali wamefanya utafiti kuhusu suala la lugha mwiko na tasfida. Aswani (2006) anaeleza kwamba mwiko ni jambo lililokatazwa katika jamii na watu wa jamii hiyo. Jamii ndiyo huamua ni mambo gani yawe mwiko.

Bakhtin (1984) katika Mwamzandi (2001) ameeleza mambo ya kingono katika jamii nyingi ni ya mwiko, hivyo basi hayazungumziwi hadharani. Inapobidi yazungumzwe, tasfida hutumika. Utafiti huu ulibaini istilahi za tasfida ambazo hutumika kuzungumzia maswala ya ngono katika jamii ya Ameru.

Barridge (1991) ameonyesha makundi nane ya lugha mwiko: yanayorejelea maswala ya ngono, maneno ya kukufuru, maneno ya skatolojia, majina ya wanyama, ubaguzi wa rangi na jinsia, maneno yanayodokeza uhusiano wa kiukoo, maneno pujufu na misimu ya kuudhi. Katika utafiti huu tulizingatia makundi matatu ambayo ni: masuala ya ngono, sehemu za siri na matusi ili kubainisha na kupambanua istilahi za mwiko za kurejelea mada hizi na kuonyesha tasfida yake na namna ambavyo istilahi za tasfida zinavyomsawiri mwanamume na mwanamke katika jamii ya Ameru.

Aswani (2006) anahoji kwamba kuna lugha ambayo inapaswa kutumiwa na watu mahsusi katika hali na mazingira fulani. Usomi huu ulionyesha hali na mazingira ya matumizi ya lugha mwiko na tasfida katika jamii ya Ameru. Takribani kila jamii ina misamiati iliyotengwa kuwa ni mwiko. Neno huchukuliwa kuwa ni mwiko iwapo linaibua hisia mbaya kwa msikilizaji, linakufuru au linaweza kuvunja imani ya wanajamii. Matusi katika lugha nyingi ni maneno yanayohusiana na uana na sehemu za siri. Matusi ni mwiko kwani si kawaida kusemwa mbele ya watu. Suala hili lilikuwa muhimu katika utafiti huu kwani tuliweza kuonyesha maneno ambayo ni matusi yanahusishwa na sehemu za siri za jinsia gani, na yanayokera zaidi yanarejelea sehemu za siri za jinsia gani.

Jay na Janschewitz (2006: 267-288) wanatathmini kwamba wanajamii wanaozungumza lugha fulani katika tamaduni mbalimbali, huelewa wakati na wapi pa kutumia maneno ya mwiko. Utafiti huu ulionyesha miktadha ya matumizi ya lugha mwiko na tasfida katika jamii ya Ameru.

Berges (1983: 123-133) na Jay na wengine (2006) wameeleza jinsi wazazi wana wasiwasi sana kutumia maneno ya ngono wakiwa na watoto. Katika usomi huu tulionyesha istilahi za tasfida ambazo wazazi wanatumia kurejelea maswala ya ngono wakiwa na watoto katika jamii ya Ameru. Jambo la kimsingi la mwanaisimu ni kubainisha ni maneno gani yanafaa katika miktadha fulani ya kijamii ili kuzungumzia maswala ya ngono, sehemu za siri na tofauti za kijinsia. Haya ni maswala ya mwiko na yanatuhusu kila siku.

Bakhtin (1984) ameeleza jinsi baadhi ya maungo ya mwili yanasawiriwa katika jamii. Ameeleza kuwa jamii zingine huonyesha maungo ya mwili hasa ya kike kwa njia ya fedheha, kama yanayokunya, yanayokojoa, yanayozaa na yanayojamiiana. Kusema mambo haya tasfida hutumika. Jambo hili lilikuwa muhimu katika utafiti huu kwani tulionyesha jinsi ambavyo maungo ya mwili husawiriwa hasa ya kike, pia tasfida ya majukumu ya sehemu za siri ilionyeshwa na jinsi ambavyo inamsawiri mwanamume na mwanamke katika jamii ya Ameru.

Nelsen (1990, katika Ndambuki, 2010) anahoji wanawake husawiriwa na majukumu yasiyoepukika kama vile: kupata hedhi na kupachikwa mimba, ilhali wanaume wanasawiriwa na majukumu yanayohitaji nguvu za mwili. Lugha ya Kiingereza husawiri mwanamke kama viumbe wa kukaa tu (*passive)* lakini wanaume ni viumbe tendaji (*active*). Pia humsawiri mwanamke kama kitu cha kula mathalani: Peremende (*sweet*) na baadhi ya vitendo kulinganishwa na mimea kwa mfano kuvunja ubikira (*deflowering*). Swala hili lilitusaidia katika utafiti huu madhali tulionyesha jinsi ambavyo wanawake wanasawiriwa na lugha mwiko na ya tasfida katika lugha ya Kimeru. Pia tulibaini taswira mbalimbali za wanaume kwa misingi ya istilahi za tasfida za sehemu za siri, na katika tendo la ngono. Fauka ya hayo tulionyesha jinsi ambavyo istilahi za tasfida zinamsawiri mwanamke kama vitu vya kula na mimea katika jamii ya Wameru.

Choti (1998) anadhihirisha wanawake ni viumbe wasio na uwezo, kwa kuzingatia lugha ya Ekegusii hasa vitenzi na methali, ilhali wanaume ni viumbe wenye uwezo na ujasiri. Suala hili lilituwezesha kutumia nadharia ya uwezo uume kuonyesha jinsi ambavyo lugha mwiko na istilahi za tasfida humdunisha mwanamke na kumtukuza mwanamume hasa katika tendo la ngono na istilahi za kurejelea sehemu za siri.

Abudi na Yieke (2011) alizingatia lugha ya Dhuluo, kwa misingi ya jazanda na misemo, alidhihirisha jinsi wanawake wanavyodunishwa kupitia kwa lugha. Katika utafiti huu, tulizingatia jazanda za istilahi za lugha ya tasfida kuhusiana na: tendo la ngono, majukumu ya sehemu za siri na istilahi za kurejelea sehemu za siri ili kubainisha jinsi ambavyo mwanamke na mwanaume wanavyosawiriwa katika jamii ya Ameru.

Jay (2003) anahoji kuwa tunapozungumzia maswala ya ngono katika miktadha mbalimbali lazima tuteue istilahi zinazofaa kwani maneno ya mwiko huonekana kukirihi katika uneni rasmi. Mathalan katika uneni wa kiliniki neno *dick*-mboo halitumiki badala yake neno *penis*-umme linakubalika. Katika utafiti huu tulibaini istilahi zinazotumika kurejelea sehemu za siri na tendo la ngono, katika miktadha mbalimbali ya mazungumzo katika jamii ya Ameru.

Wardhaugh (1986: 23) ameeleza kila utamaduni una lugha ya tasfida. Hivyo basi, katika utafiti huu tulijikita katika matumizi ya lugha ya tasfida inayotumika kurejelea sehemu za siri, tendo la ngono na majukumu ya sehemu za siri. Sunderson (1999: 259) anahoji kwamba lugha ya tasfida hutumika kuonyesha unyenyekevu. Katika utafiti huu tulibaini dhima ya tasfida katika jamii ya Ameru na kuonyesha jinsi ambavyo inasawiri jinsia.

Hai-Long (2008) anasisitiza kuwa lugha na utamaduni ni mambo ambayo hayawezi kutenganishwa na tasfida ni kitambulisho cha utamaduni. Ni kuhusiana na suala hili ambapo tuliweza kuonyesha baadhi ya utamaduni wa jamii ya Ameru kupitia kwa lugha ya tasfida mathalan kumtukuza mwanamume na kumtweza mwanamke. Pia tulionyesha baadhi ya majukumu ya mwanamume na mielekeo ya wanajamii kuhusiana na uana. Mintarafu ya hayo matumizi ya tasfida kutoka utamaduni moja hadi mwingine ni tofauti kwa sababu za kihistoria, kaida za jamii na dini.

Msingi wa Nadharia

Katika utafiti huu tulitumia nadharia ya: Uwezo Uume na Uchanganuzi Hakiki Usemi.

Nadharia Ya Uwezo Uume

Connell (1982) anasema dhana ya Uwezo Uume iliasisiwa kwa mara ya kwanza katika ripoti za usomi kuhusiana na ubaguzi wa kijamii katika shule za upili nchini Australia kisha ikapambanuliwa na Connell (1987) ambapo alisisitiza Uwezo Uume ni hali ya kuhalalisha uwezo wa wanaume dhidi ya wanawake katika jamii. Mihimili ya nadharia hii ni: itikadi za jamii, uwezo, mamlaka na utamaduni na mazingira.

Nadharia ya Uwezo Uume ilitupatia utambuzi muhimu juu ya umuhimu wa dhakari kama kielelezo cha mamlaka ya mwanamume juu ya mwanamke. Aidha, ni sehemu muhimu iliyojenga umaizi wetu katika kutambua jinsi ambavyo kiungo hiki cha uzazi hutumiwa na jinsia ya kiume ili kudhihirisha ubabe dume wao. Tulizingatia istilahi za tasfida ambazo hupewa kiungo hiki na majukumu ya kiungo hiki katika jamii ya Ameru. Kwa upande wa mhimili wa mamlaka Donaldson (1993) anahoji kwamba mtazamo wa Uwezo Uume hubainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Wazo "Mwanamume" lipo kwa misingi ya kubaolojia ilhali "uume" hutokana na: mielekeo, imani na matarajio ya kijamii. Hivyo basi, 'uume' huzaliwa na kukuzwa na utamaduni na huhalalishwa kupitia kwa lugha.

Kuhusiana na muhimili wa utamaduni, Knights (1999) na Harwood (2000, katika Izugbara, 2005) wanauona uume kuwa unakuzwa na kuendelezwa na tamaduni za jamii. Kwa sababu tasfida ni kioo cha utamaduni, utafiti huu ulionyesha jinsi lugha ya tasfida kuhusiana na masuala ya sehemu za siri, tendo la ngono na majukumu ya sehemu za siri inavyoonyesha ubabe dume. Kuhusu muhimili wa uwezo, Izugbara (2005: 13) anasema, umbo la dhakari la ubenuzi, na hali ya kutokuwa na haya ikishirikishwa na uwezo wa dhakari kuwa ngumu, kubwa thabiti na yenye nguvu wakati wa mchechemo ni dhihirisho kuwa dhakari ina uwezo. Shahawa ambayo dhakari hutoa wakati wa kujaamiana huonekana kama sumu ambayo humdhoofisha mwanamke. Jambo hili lilibanika katika istilahi za tasfida za uume na istilahi za kurejelea tendo la ngono. Suala hili linamdunisha mwanamke.

Connell (2005) anasema kuna mhimili wa itikadi za kitamaduni ambazo hubainisha: aula, uweza, nguvu, uhodari na uhayawani wa mwanaume ni kielelezo chake cha mamlaka. Fauka ya hayo: utendakazi wa viungo vya uzazi, upenyezi wa dhakari wakati wa kujaamiana, kuwa na uhusiano wa kingono na zaidi ya mwanamke mmoja nje ya ndoa, ushari wa kimapenzi na sauti nzito ni sifa mwafaka zenye kumtambulisha mwanamumne tofauti na wasiomiliki dhakari. Mawazo haya pia yalibainika kupitia lugha ya tasfida ya sehemu za siri na tendo la ngono miongoni mwa mwanamume.

Izugbara (2005) anaendelea kusema kuwa dhakari hutumika kama chombo cha kumzusha hadhi mwanamke kwa sababu hii dhakari ni asili ya uanaume, silaha ya kumwezesha mwanamume kuwa mshindi katika ushindani wa kijinsia. Maana yake na umuhimu wake huhalalishwa katika tendo la ngono. Swala hili pia lilijitokeza katika istilahi za tasfida za tendo la ngono na istilahi za tasfida za uke.

Kwa muhtsari nadharia hii imejikita katika mambo manne muhimu ambayo hutawala matarajio na mielekeo ya jamii kuhusu mwanaume. Itikadi za jamii, uwezo, mamlaka, utamaduni na mazingira. Nadharia hii ilikuwa mwongozo thabiti katika kutathmini, uwezo wa mwanamume katika jamii ya Ameru kupitia istilahi za tasfida kuhusiana na tendo la ngono, sehemu za siri na majukumu ya sehemu za siri.

Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi

Waasisi wa nadharia hii ni Ruth Wodak, Teun van Dijk na Norman Fairclough. Nadharia hii imekuwa muhimu sana katika uchanganuzi wa usemi ambao unahusiana na masuala ya uwezo na vile vile ubaguzi. Katika uchanganuzi wa matini nadharia hii huangazia mihimili muhimu ifuatayo: itikadi, uwezo na uhakiki. Itikadi ni imani pendwa katika kipindi maalumu cha historia. Uwezo ndicho kile ambacho huleta tofauti katika uhusiano wa jinsia, makundi

na kadhalika. Uhakiki unahusiana na kutathmini pasipo na kuwa na mapendeleo (Wodak, 2001).

Uchanganuzi wa Data

Istilahi za Umme (*Muthirinya*)

Tuligundua kuna istilahi za kurejelea umme, nazo zilikuwa *mujiji, nkai, nchabu na muthirinya*. Neno ambalo lilikuwa na asilimia ya juu ni *Nkai* (makende) ambalo asilimia yake ilikuwa sabini. *Mujiji* linatokana na neno *mwiji*-mvulana ambaye hajapashwa tohara. Ni mwiko kumrejelea mwanamume ambaye amepashwa tohara kama *mwiji* badala yake ni *munthaka.*

Jedwali 1: Istilahi za umme

Kimeru	Kiswahili	Umaratokezi %
Nkai	Makende	70
Muthirinya	Dhakari	20
Nchabu	Govi	5
Mujiji	Dhakari	5

Asili: Nkumbo (2013)

Istilahi *nkai* ndiyo ilikuwa na asilimia ya juu ya umaratokezi. Hutumika kurejelea sehemu za siri za wanaume kwa jumla.

Istilahi za Tendo la Ngono (*kuthicana, Kubandana, Kurijana)*

Istilahi hizi: *kuthicana, kubandana* na *kurijana* ndizo za mwiko za kutaja wakati unaporejelea tendo la ngono. Neno ambalo lilikuwa na umaratokezi wa juu *ni kuthicana*. Hii ni kwa sababu ndiyo istilahi ambayo hurejelea tendo la ngono baina ya binadamu. Istilahi *kubandana ni* ya jumla hurejelea tendo la ngono baina ya wanyama na binadamu ingawa haitumiki sana. *Kurijana* ni istilahi ambayo ni ya tasfida. Katika jamii ya Ameru siyo watu wote ambao wana ruhusa ya kushiriki tendo la ngono. Wanaopaswa kushiriki ni wale tu wamefunga ndoa. Ndiposa istilahi za kurejelea hali hii huwa ni mwiko kutaja. Hata hivyo, kaida hii imevunjwa na baadhi ya wanajamii ambao hushiriki ngono hata kabla hawajafunga ndoa.

Jedwali 2: Istilahi za tendo la ngono

Kimeru	Kiswahili	Asilimia ya umaratokezi
Kuthicana	Kujamiiana	80
Kubandana	Kujamiiana	10
Kurijana	Kujamiiana	10

Asili: Nkumbo (2013)

Istilahi *kuthicana* ndiyo ilikuwa na umaratokezi wa juu. Hii ni kwa sababu inarejelea tendo la ngono baina ya binadamu. Istilahi *kurijana* inaashiria hali ya kula hivyo basi ikitumika huwa inaficha siri. Kwa sababu ya matumizi yake na wanajamii imekuwa ni mwiko.

Maneno ambayo ni Matusi

Maneno ambayo yaliorodheshwa kuwa ni matusi ni: *ncabu, kiino, mukundo, mpene, kuru, nyakwe na king'ura*. Tuligundua maneno haya huwa ni matusi kwani yalitumika wakati wanajamii wamekasirika. Pia ni maneno ambayo hayasemwi hadharani. Mtu akiwa amekasirika huweza kutumia baadhi ya maneno haya badala ya kuzua vita. Utafiti uligundua matusi yanayorejelea sehemu za siri za wanawake ni mengi kuliko yale yanayorejelea

sehemu za siri za wanaume. La kushangaza ni kuwa hata wanawake walitumia hayo maneno kuwatusi wanawake wengine. Matusi waliyotumia ni yale yanayorejelea sehemu za siri za wanawake ni: *kiino, mpene* na *king'ura*. Jambo hili linadhihirisha kuwa maneno yanayohusu jinsia ya kike ndiyo yenye kero zaidi.

Jedwali 3: Istilahi za Matusi

Kimeru	Kiswahili	Asilimia ya umaratokezi
Ncabu	Govu	18
Kiino	Kuma	25
Mukundo	Mkundu	23
Mpene	Kuma	5
King'ura	Kuma	5
Kuru	Mbwa	12
Nyakwe	Mzazi wa kike	12

Asili: Nkumbo (2013)

Istilahi za Tasfida kuhusiana na Sehemu za Siri

Baada ya kudhihirisha matumizi ya lugha mwiko, sehemu hii itapambanua tasfida ya maneno hayo. Baadhi ya istilahi za tasfida zinaweza kuwa za mwiko kwa sababu ya matumizi yake kila wakati, hivyo basi kujulikana na wanajamii wengi.

Tasfida ya Umme (*muthirinya)*

Tuligundua kuna istilahi kadhaa za tasfida za kurejelea umme, utafiti uligundua kuna istilahi kumi za kurejelea dhakari.

Jedwali 4: Istilahi za tasfida ya umme

Kimeru	**Kiswahili**	**Jinsia inayotumia**	**Umri- miaka**	**% umaratokezi**
Muti	Mti	Kike na kiume	18-50	30
Mumutani	Kifaa cha kudunga	Kike	18-50	2
Mugugu	Mkia	Kike na kiume	18-35	7
Muntancune	Kutotosheka	Kiume	18-50	15
Ncuguma	Rungu	Kike na kiume	18-35	2
Muugwi	Mshale	Kiume	35-50	3
Munyamu	Mnyama	Kike na kiume	18-50	8
Urume	Umme	Kike	18-50	3
Mununtha	Mkia	Kike /kiume	18-50	6
Mukunguru	Mwiba	Kiume	18-35	6
Chuma	Chuma	Kiume	18-50	8
Maiga	Mawe	Kiume/kike	18-50	10

Asili: Nkumbo (2013)

Taswira ya Mti (*muti*)

Istilahi hii ilikuwa na asilimia thelathini. Ni neno ambalo linatumika na takribani kila mwanajamii. Umme unalinganishwa na mti kwa sababu ya maumbile yake. Istilahi hii ni maarufu kwa wavulana waliopashwa tohara, wale ambao hawajapashwa tohara wana istilahi za kutumia kurejelea umme kama vile, *muthirinya* ambayo ni mwiko. Katika hali halisi mti huwa na manufaa kama vile ya ujenzi. Mwananamume akipashwa tohara katika jamii ya Ameru huwa ana idhini ya kuoa na kujenga familia yake pia anapaswa kutoa ulinzi wa familia na jamii kwa jumla. Umme unalinganishwa na mti kwa sababu wanajamii wanaamini

kuwa una manufaa kama yale ya mti halisi. Kwa kawaida miche ya miti hupandwa shimoni. Hali hii inaashiria kushiriki ngono, ndiposa katika jamii ya Ameru wavulana waliopashwa tohara huishi kuwasaka wasichana ili washiriki ngono na wao. Jambo hili huwa ni sifa kubwa kwa wavulana hawa.

Taswira ya Kudunga (*mumuntani)*
Neno hili lilikuwa na asilimia mbili ya umaratokezi. Linatumika sana miongoni mwa jinsia ya kike. Utafiti uligundua ni kutokana na ule uwezo wa dhakari wa kuvunja ubikira na kujipenyeza ndani mwa uke wakati wa tendo la ngono, ndio maana umme ukapewa jina hili. Kifaa ambacho kina uwezo wa kudunga huwa na ncha kali na hutiwa makali. Wakati wa tohara kitendo cha kutahiri hulinganishwa na kutia umme makali ili uweze kutekeleza jukumu la tendo la ngono.

Taswira ya Mkia (*mugugu, mununtha*)
Kulikuwa na istilahi mbili ambazo zilionyesha dhana ya mkia. Istilahi hizi zilikuwa ni *mugugu* asilimia saba na *mununtha* asilimia sita. Istilahi hizi zilitumika miongoni mwa jinsia zote. Istilahi hii inatokana na maumbile ya dhakari ya kuwa kama mkia. Kwa kawaida mkia huwa mgumu, umme hulinganishwa na mkia ambao umelemaa ndio maana sio mrefu. Hali hii inaonyesha wanaume waliumbwa kama wanyama walio na mikia kama wanyama wengine. Dhana hii inaashiria uhayawani wa wanaume.

Dhana Kutotosheka (*muntancune*)
Hii ni dhana ambayo inaonyesha hali ya kutotosheka baada ya kutenda jambo fulani. Katika maisha ya binadamu mtu akifanyiwa jambo zuri huwa anashukuru. Wale ambao hawashukuru hurejelewa na dhana hii ya '*muntancune*'kuonyesha pengine hawajatosheka. Dhakari imepewa jina hili kwa sababu ya uchu wake ambao daima hauishi. Baada ya tendo la ngono, ashiki ya mwanamme hurejea tena upesi. Hali hii humfanya kushiriki ngono na wanawake wengi ili angalau atosheke. Dhana hii ilikuwa na asilimia kumi na tano, na hutumiwa na jinsia ya kiume. Inatokana na imani za wanajamii za kuhalalisha baadhi ya matendo ya wanaume kwa mfano, kuwa na wanawake wengi wa halali na nje ya ndoa.

Taswira ya Rungu (*Ncuguma*)
Ni istilahi ambayo inatumika na jinsia zote. Ilikuwa na asilimia mbili. Rungu ni ala ya kivita. Dhakari imepewa jina hili kwa sababu ya maumbile yake yaliyo kama ya rungu. Rungu huchongwa kutoka kwa miti. Dhana hii inaonyesha kupashwa tohara. Rungu hutumika kama ala ya vita. Jambo ambalo linaonyesha silaha ya mwanamume dhidi ya mwanamke katika tendo la ngono.

Taswira ya Mshale (*Muugwi*)
Ni istilahi inayotumika miongoni mwa jinsia ya kiume. Neno hili lilikuwa na asilimia tatu ya umara tokezi. Linatokana na uwezo wa dhakari wa kumdunga mwanamke mimba. Wakati mwanamke amepata mimba hulinganishwa na mshale uliofuma sawasawa. Mshale ni ala ya kivita hivyo dhakari imelinganishwa na mshale kwa sababu ya maumbile yake. Tohara ya wavulana huhusisha kukatwa kwa govi. Kitendo hiki husawiriwa katika jamii ya Ameru kama kutia makali mshale ili ukifuma (tendo la ngono) uweze kumdhoofisha adui kabisa. Hali hii inaonyesha urejeleo wa majukumu ya umme katika kuendeleza uwezo uume.

Taswira ya Mwiba *(mukunguru*)
Ni istilahi inayotumika miongoni mwa jinsia ya kiume. Ilikuwa na asilimia sitini. Mwiba ni aina ya mmea ambao hudunga. Dhakari imepewa jina hilo kutokana na uwezo wake wa

kudunga mwanamke mimba na kuvunja ubikira wake. Mti ambao huwa na miiba ni ufananisho ambao unadhihirisha kuwa mwanamume sharti kujihami na silaha zake ambazo zinafananishwa na mwiba, katika kulinda jamii. Pia inaonyesha uimara wa dhakari katika tendo la ngono.

Taswira ya Chuma na Mawe *(Cuma, maiga*, *maune*)
Istilahi hizi zinadokeza maana sawa. Chuma ni kifaa ambacho ni kigumu mno na hutumika vitani. Istilahi chuma ilikuwa na asilimia nane na mawe asilimia kumi. Hivyo basi, umme unalinganishwa na mawe na chuma kwa sababu ya uwezo wake kuwa mgumu mithili ya chuma wakati wa tendo la ngono ili kumdhoofisha mwanamke. Dhana hii inadokeza kwamba wakati wa tohara mwanamume sharti awe mgumu mithili ya mawe, asionyeshe hisia za uchungu wala maumivu kwani dalili hizi ni ishara ya uoga. Katika jamii ya Ameru wanaume ni viumbe imara kiasi kwamba hawatingiziki wala kushtuliwa. Dhana hizi zinaonyesha uthabiti wa wanaume wakilinganishwa na wanawake.

Dhana ya Umme (*urume*)
Ni istilahi ambayo ilikuwa na asilimia tatu. Inadokeza hali ya kuwa mwanamume kwa sababu ya sehemu za siri za mwanamume. Linatumika miongoni mwa jinsia zote. Hali hii ni ya kibaolojia hivyo basi, aliye na uume anarejelewa kama *murume* katika jamii ya Ameru. Uume uhusishwa na mwanaume kudhibiti nafsi na hadhi yake.

Tasfida ya Tendo la Ngono
Maneno ambayo ni mwiko yakurejelea tendo la ngono ni*: kuthicana, kubandana na kurijana.* Tuligundua kuna istilahi kumi na tano za kurejelea dhana ya tendo la ngono.

Jedwali 5: **Istilahi za tasfida za kurejelea tendo la ngono**

Kimeru	**Kiswahili**	**Jinsia/inayotumia**	**Asilimia ya umara tokezi**
Kurijana	Kula	Zote	10
Kunywa mbaki	Kunywa ugoro	Zote	6
Kunywa mwonyo	Kunywa mchanga	Kiume	4
Kugaana gitunda	Kugawana tunda	Zote	7
Kibikunda	Kunywa	Kiume	6
Gugi ya mugwi jumwe	Kazi ya mshale moja	Kiume	3
Kumaama	Kulala	Zote	3
Kuringwa kasio	Kudungwa kisu	Zote	9
Kuthithania	Kufanyana	Kiume	5
Kwonana kimwiri	Kuonana kimwili	Kiume	10
Gukundurira rucoro	Kufungua ugoro	Kiume	10
Kumuntana	Kudunga	Kiume	7
Kuratha	Kufuma	Kiume	8
Kurumwa thiguku	Kupewa kichakaa	Kiume	4
Kurumwa ngakua	Kupewa baridi	Zote	8

Asili: Nkumbo (2013)

Jedwali hili linaonyesha istilahi za tendo la ngono ambazo ni za: tasfida, jinsia wanaozitumia na umaratokezi wa kila istilahi. Kulingana na utafiti huu ni wazi kwamba hamna istilahi ambazo zinatumiwa na jinsia ya kike pekee kama ilivyo katika jinsia ya kiume.Tuligundua istilahi nyingi zinatumiwana wanajamii kati ya miaka kumi na nane hadi hamsini. Istilahi

ambazo zinatumiwana wanajamii kati ya miaka thelathini na mitano hadi hamsini ni mbili nazo ni: kazi ya mshale mmoja na kudungwa kisu.

Kula (***kurijiana***)
Tulibaini istilahi hii ilikuwa na asilimia kumi ya umaratokezi. Istilahi hii hutumika miongoni mwa jinsia zote. Inaonyesha wakati wa tendo la ngono dhana ni kwamba watu wanakula mithili ya kula chakula. Hivyo basi tendo la ngono ni kukulana. Mtafiti aligundua kwamba wanawake ndio 'huliwa' ilhali wanaume ni walaji. Kila mwanajamii anatumia istilahi hii kurejelea tendo la ngono.

Kula Ugoro (*kuria mbaki*)
Ilikuwa na asilimia sita ya umaratokezi. Mtafiti alibaini tendo la ngono ni kama kupewa tumbako. Tulibaini kwamba wakati mvulana anamtongoza msichana huwa anasema '*kundia mbaki'* nipe ugoro. Hivyo basi iwapo atakubaliwa huwa anavuta tumbako. Msichana analinganishwa na tumbako.Tumbako ni dawa ya kulevya ambayo hutumiwa kupumbaza. Pia tumbako hutumiwa kama ya burudani. Dhana ni kwamba mwanamke ndiye hutoa burudani kwa mwanamme katika tendo la ngono. Istilahi hii hutumika miongoni mwa wanaume. Dhana hii pia ina uhusiano na kufunguliwa ugoro. Jinsi ambavyo ugoro hufungwa kwa kutumia majani ya ndizi yaliyo kauka *gukundurira rucoro.* Hivyo basi wanawake huwafungulia ugoro wanaume kuashiria kushiriki tendo la ngono.

Kugawa Tunda (*kuugana Gitunda*)
Hii ni istilahi ambayo inaonyesha tendo la ngono ni kama kugawanya tunda. Hivyo basi, wote wanaoshiriki wanagawanya tunda ili kila mmoja afurahie sehemu yake. Inaonyesha tendo la ngono ni dhana ya kula. Kishazi hiki kilikuwa na asilimia saba ya umaratokezi. Neno hili lina mizizi yake kutoka Bibilia takatifu kwani Adamu na Hawa walilila tunda ambalo lilikatazwa na mwenyezi Mungu.

Kunywa (*kubikunda*)
Hii ni dhana ambayo inaashiria kunywa kitu ambacho ni majimaji. Hivyo basi, katika tendo la ngono wanaume huonyeshwa kama wao ndio wanywaji ilhali wanawake ndio walio na maji ya kunywewa. Dhana hii ina uhusiano na kunywa maji yenye chumvi (*mwonyo*).

Kulala (*kumaama*)
Katika tendo la ngono washiriki huwa wanalala pamoja. Hivyo basi tasfida inayotumika ni kulala. Ilikuwa na asilimia tatu. Ni dhana inayotumiwa na jinsia zote na watu wa umri zaidi ya miaka kumi na nane. Tuligundua hii ndiyo istilahi ya kijumla inayorejelea tendo la ngono.

Kazi ya Mshale Moja (*Ngugi ya mugwi jumwe*)
Tendo la ngono linalinganishwa na kazi ya mshale mmoja. Dhana hii hutumika miongoni mwa wanaume kati ya miaka 36-50. Mshale ni ala inayotumika katika vita. Dhana hii inatokana na maumbile ya dhakari ambayo ni kama mshale na huwa ni moja. Istilahi hii ina uhusiano na dhana ya kudunga kwa kutumia kisu. Hivyo basi, mwanaume ndiye hudunga. Dhana ya kudungwa hutumika miongoni mwa wanaume. Iwapo mwanamke atapata mimba huwa ni mshale uliofuma sawasawa.

Kudungwa kwa Kisu (*kuringwa kasio*)
Dhana hii inatokana na tohara ya wanaume kwamba wanapotahiri huwa ni kama kisu ambacho kinatiwa makali ili kiweze kudunga sawasawa. Hutumika miongoni mwa wanaume waliopashwa tohara na lilikuwa na asilimia tisa ya umaratokezi.

Kuonana Kimwili (*kuonana kimwiri*)
Katika tendo la ngono washiriki huwa wanaonana kimwili, hii ni kwa sababu huwa wako uchi. Kila mmoja anaweza kuona uchi wa yule mwingine. Istilahi hii ilikuwa na asilimia kumi. Hutumika sana miongoni mwa wanajamii.

Kufanyana *(kuthithania*)
Ni istilahi ambayoina asilimia tano ya umaratokezi. Ni hali ya kufanyana wote wanaoshiriki ngono inadhaniwa wanafanyana. Inatokana na kitenzi fanya. Istilahi hii inatumika na jinsia zote.

Kupewa Kitu Kilichochakaa *(kurumwa thiiguku*)
Hii ni dhana ambayo inaonyesha wanaume ndio wanapewa kitu kilichochakaa. Kuchakaaa hutokana na istilahi ambayo ni ya kitu ambacho kimetumika kwa miaka mingi hivyo kupoteza rangi yake. Uke unalinganishwa na kitu kilichochakaa kwa sababu ya kushiriki ngono. Istilahi hii ina asilimia nne na hutumika miongoni mwa wanaume.

Kupewa Baridi (*kurumwa ngakua*)
Hii ni dhana ambayo inaonyesha katika tendo ngono huwa ni mwanamme anayepewa baridi ili kutuliza ashiki yake. Neno hili linatumika na jinsia zote. Lilikuwana asilimia nane ya umaratokezi.

Hitimisho

Katika makala hii tulitathmini istilahi za tasfida ambazo zinaonyesha usawiri wa jinsia katika jamii ya Ameru. Tulizingatia istilahi ambazo zinaonyesha hali hii kwa kuzingatia istilahi za tasfida za sehemu za siri na tendo la ngono. Tulifanya hivi kwa kuongozwa na nadharia za Uwezo Uume na Uchanganuzi Hakiki wa Usemi katika kuchanganua istilahi za tasfida zinazotumika kurejelea sehemu za siri za wanaume na tendo la ngono. Uume hutokana na mielekeo, imani na matarajio ya utamaduni wa jamii. Hivyo basi uume huzaliwa na kukuzwa na utamaduni na huhalalishwa na jamii nzima.

Imebainika kwamba sura ya mwanamume katika jamii haitokani na ombwe tupu au wanavyojifikiria wanaume bali sura hizo hujengwa kutokana na matarijio ya kiitikadi na kitamaduni kuwahusu- ni kutokana na matarajio haya ambapo baadhi ya sifa husisitizwa, kwa mfano; stahamala, ubabe na ukatili katika kutenda bila kujali iwapo vitendo hivyo vitaleta maangamizi au vurugu katika jamii. Swala hili limebainishwa kupitia lugha ya tasfida ya sehemu za siri za wanaume na katika tendo la ngono kwani istilahi ambazo zinatumika zinamkuza mwanaume na za kike zinamtweza mwanamke. Pia istilahi hizi zinaonyesha jukumu la mwanaume la kulinda jamii. Ndiposa istilahi za sehemu za siri zimeundwa kwa kufananisha na zana za kivita.

Dhakari imetawazwa na umuhimu wa uhai na ufu. Matokeo muhimu huhusishwa na amali ya dhakari na upenyezi wake katika kupoteza ubikira na kutia mimba, hali hii huitukuza dhakari. Suala hili lilibainika katika istilahi za tasfida za kuvunja ubikira na kupachika mwanamke mimba kwani istilahi hizi zilionyesha hali ya mwanaume kumdhoofisha mwanamke kabisa.

Itikadi za kitamaduni ambazo hubainisha: aula, uwezo, nguvu, uhodari na uhayawani wa mwanaume, kielelezo chake cha mamlaka, utenda kazi wa viungo vya uzazi, upenyezi wa dhakari, kuwa na uhusiano wa kingono na zaidi ya mwanamke mmoja nje ya ndoa ushari wa kimapenzi, huchukuliwa kama sifa mwafaka zenye kumtambulisha mwanaume tofauti na wasiomiliki dhakari. Hali hizi pia zilibainika kupitia maneno ya tasfida ya sehemu za siri za wanaume.

Istilahi za tasfida za dhakari zimeonyesha kwamba dhakari hutumika kama chombo cha kumzusha hadhi mwanamke katika jamii ya Ameru. Kwa sababu hii dhakari ni asili ya 'uume' silaha ya kumwezesha mwanaume kuwa mshindi katika ushindani wa kijinsia. Maana yake na umuhimu wake huhalalishwa katika tendo la ngono na sifa zake muhimu zenye kuakisi matarajio ya jamii juu ya mwanamume.

Vitenzi vinavyotumika katika istilahi za tendo la ngono ni vya utendaji vya kuonyesha mwanaume ndiye mtendaji katika tendo la ngono naye mwanamke ni tuli. Mtafiti alibaini kuwa katika tendo la ngono istilahi nyingi ni zile za kula na kunywa hivyo basi ni kama chakula ambacho huliwa kwa mfano tunda na tumbako.

Pia tuligundua katika tendo la ngono ni kama washiriki wako vitani, ndiposa istilahi kama kudungwa na kufumwa mshale hutumika. Yule anayeshinda vita hivi ni mwanamume kwani yeye ndiye aliye na ala za kivita kama vile kisu na mshale. Mwanamke akipata mimba mshale huwa umefuma sawasawa.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu tumedhihirisha mtazamo wa jinsia ya kiume hubainishwa kuwa na thamani ya juu. Hivyo basi, itikadi za kiume na muundo wa kiuwezo humpa mwanamume uwezo juu ya mwanamke. Lugha kama kioo cha utamaduni wa jamii huhusika katika kudhihirisha tofauti za mahusiano ya kiuwezo baina ya mwanamume na mwanamke. Hali hii huendeleza kumdhalilisha mwanamke na kumtukuza mwanamume. Istilahi zingine zinaonyesha hali ya dharau dhidi ya mwanamke mathalan kuchakaa na donda ndugu.

Baadhi ya istilahi zinaonyesha jukumu mojawapo la mwanamke katika jamii ya Ameru ni kutoa burudani kwa mwanamume. Hii inaonyeshwa katika istilahi kama vile, baridi na ugoro. Katika sehemu hii tumechanganua istilahi za tasfida kuhusiana na sehemu za siri. Kusudi kubwa lilikuwa kutathmini jinsi ambavyo jinsia inavyosawiriwa katika jamii, kwa kuzingatia nadharia ya Uwezo Uume na Uchanganuzi Hakiki wa Usemi, na kubainisha taswira ya istilahi za sehemu za siri za jinsia ya kiume na tendo la ngono. Idadi ya istilahi tulizoshughulikia ni sehemu ndogo ya hazina kubwa ya istilahi za tasfida miongoni mwa Ameru. Kwa mujibu wa matokeo haya tunatoa rai, kuwa istilahi za mwiko na tasfida zishirikishwe vilivyo katika kujenga na kukuza usawa wa kijinsia.

Marejeleo

Abudi, M. & Yieke, F. (2011) *Language, Gender and power relations*. Unpublished MA Thesis. Egerton University, Kenya.

Allan, K. B, K. (1991) *Euphemism and dysphemism*. New York: Oxford University Press.

Aswani, B., Kimani, N., & Mwihaki, A. (2006*) Isimujamii*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Berges, E., Neidebach, S., & Rubin, B. (1998*) Children and sex: The parent speaks*. New York: Facts on file.

Choti, A. (1998) *The linguistic portrayal of the Gusii woman*. Unpublished MA thesis, Egerton University, Kenya.

Connell, R.W. (2005) *Masculinities* (2nd Edition). Berkeley, CA: University of California Press.

Connell, R.W. (1987). *Gender and power*: *Society, the person and sexuality politics*. Sydney Boston: Allen and Unwin.

Connell, R.W. (1982) *Ockers and discomanics*: *A discussion of sex, gender and secondary schooling* (2nd Edition). Stanmone N.S.W: Inner City Education Centre.

Donaldson, M. (1993) What is hegemonic masculinity: Theory and society. *Springer, 22* (5): 643-687.

Hai-long, H. (2008*) Intercultural study of euphemism in Chinese and English* [on-line] Retrieved June 6, 2012, from http://www.linguist.org.on/doc/su200808/su2008/0810.pdf

Izugbara, C. (2005) Hypothesis on the origin of hegemonic masculinity. *Sexuality in African Magazine, 2* (1), 13-14.

Jay, T. (2003) *The psychology of language*. NJ Prentice Hall: Upper Saddle River.

Jay, T. King, K. & Duncan, D. (2006) Memories of Punishment for Cursing. *Sex Roles, 32*, 123-133.

Mwamzandi, I, Y. (2002) *Usemezano katika taarabu*.Unpublished Phd thesis. Egerton University, Kenya.

Ndambuki, J. M. (2010) *Discursive representation of women's needs and interests*. Unpublished PhD Thesis, University of Witwaterrand, South Africa.

Nkumbo, D. (2013) *Lugha katika muktadha: Dhima ya tasfida katika Jamii ya Ameru*. Unpublished MA thesis, Laikipia University, Kenya.

Riro, M.S. (2006) *Usawiri wa mwanamume katika nyiso za jando miongoni mwa Abakuria*. Unpublished MA Thesis, Egerton University, Kenya.

Sanderson, P. (1999) *Using news paper in the classroom*. UK: Cambridge Universiry Press.

Wardhaugh, R. (1986) *An introduction to sociolingustics*. UK: Blackwell.